C. Matumizi ya mfumo wa utumiaji wa kukadiria hali za kikazi za wakulima wadogo/wafanya kazi

Zana hii inajumuisha mfuatano wa maswali ambayo wagawaji wanaweza kutumia ili kuchagua vigezo vya kukadiria hali katika mashamba madogo yanayozia bidhaa kuambatana na viwango vya kazi vilivyowekwa kwenye mfumo wa utumiaji sehemu A.2. Zana imenuiwa kuwawezesha wagawaji kutambua pahali pa kuanzia au msingi ambao watatumia kupanga hatua zitakazohitaji kuchukuliwa ili viwango vifikie vigezo vilivyoelezwa katika sehemu A.2.

C.1 Utangulizi

Wagawaji (mara nyingi wanajulikana kama 'wanunuzi' katika mwongozo huu) wanahitaji njia fulani za kuchagua vigezo vya kukadiria hali za kikazi kwenye mashamba madogo ili kuibua mpango wa hatua za dharura. Zana hii inajumuisha orodha ya maswali yanayoweza kutumiwa kwa lengo hilo. Kila swali limetolewa kutoka kwenye mistari ya alama ya mfumo wa utumiaji (**zana za kazi sehemu A**). Inapowezekana, maswali haya yameachwa wazi ili kuepuka majibu ya ndio/la. Hii inapaswa kuwawezesha wanaojibu maswali kutoa habari kamilifu zaidi na, kwa hivyo mhojaji kupata picha kamilifu ya hali ya mwenye kujibu maswali.

Majibu kwa maswali hayo yanaweza kutoka kwa rekodi na uchunguzi wako mwenyewe. Hata hivyo, mara nyingi habari hizo huenda zikahitajika kutoka kwa wakulima wadogo/wafanya kazi wenyewe. Jua kwamba wafanya kazi ni pamoja na wanafamilia ya mkulima mdogo na waajiriwa. Mwongozo wa kukadiria mahitaji na vipaumbele vya wakulima wadogo unapatikana katika **zana za kazi, sehemu B**. Maswali hayo yanaweza kuhitaji marekebisho ili kufaa hali za kampuni yako.

Vifupisho

PPE - Vifaa vya kujikinga binafsi.
SH - Mkulima mdogo.
SHE - Mkulima mdogo mwajiri.
TU - Chama cha wafanya kazi.

C. 2 Ajira inachaguliwa kwa hiari ya mtu mwenyewe

- Je, ni nyaraka zipi za SH/wafanya kazi, ikiwa ziko, zinazohifadhiwa nawe/SHE au mlanguzi (k.m. stakabadhi za kijitambulisha au pasi)?
- Je, kuna SH/wafanya kazi wo wote wanaodaiwa nawe/SHE au mlanguzi?
- Je, kuna SH/wafanya kazi wo wote wanaotoswa faini kwa sababu yo yote ile? Ikiwa ndio, je ni kwa nini?
- Je, ni kwa vipi mwendo wa SH/wafanya kazi umezuiliwa ndani ya mashamba, ikiwa mwendo umezuiliwa?
- Je, SH/wafanya kazi wanaripoti udanganyifu au kushurutishwa katika mapatano ya kazi au uajiri?

C. 3 Uhuru wa kushirikiana na wengine na haki ya makubaliano ya pamoja zinaheshimiwa?

- Je, unalinda vipi uhuru wa SH/wafanya kazi wa kuanzisha au kujiunga na mashirika na vyama vya wafanya kazi wanavyopenda pamoja na kushiriki katika shughuli za makundi hayo?
- Je, wewe/SHE mnahakikisha vipi kwamba SH/wafanya kazi wanaweza kukubaliana kwa pamoja bila ya kuogopa kisasi?
- Je, kiwango chako cha SHE cha utambuzi wa uwakilishaji husika wa TU kwa SH/wafanya kazi ni kipi?
- Je, kiwango cha SH/wafanya kazi cha utambuzi na maarifa ya kuwepo kwa uwakilishi wa TU ni kipi?
- Je, SH/wafanya kazi ni wanachama wa vyama vya wafanya kazi au mashirika mengine yapi?
- Je, ni wapi ambapo wawakilishi wa mashirika au TU ya SH/wafanya kazi wanakutana?
- Je, habari hii inapitishwa vipi (k.m. ilani zilizowekwa katika vituo vya kukusanya bidhaa)?

C. 4 Hali za kikazi ni salama na safi

- Je, hali ya vifaa/nyenzo walizopewa SH/wafanya kazi iko vipi (k.m. mwangaza na halijoto ya kutosha na hewa safi katika nyenzo za kupima ubora wa bidhaa)?
- Je, wewe/SHE mnashughulikia vipi magonjwa yanayosababishwa na hali za kazi yanayoripotiwa na SH/wafanya kazi?
- Je, ukaguzi wa kiafya ulioelezwa unafanya vipi kwa SH/wafanya kazi (k.m. ni nani anayetoa huduma hizo na mara ngapi)?
- Je, majeraha/ajali ndogo zinashughulikiwa vipi kwenye mashamba ya SH (k.m. je, wana sanduku la huduma ya kwanza)?
- Je, SH/wafanya kazi wamejizoesha vipi na sanduku la huduma ya kwanza?
- Je, ajali katika mashamba ya SH zinarekodiwa vipi (k.m. katika kitabu cha kumbukumbu za ajali)?
- Je, SH/wafanya kazi wana utambuzi upi kwamba wanapaswa kurekodi ajali?
- Je, SH/wafanya kazi wana uwezo wa kutumia PPE bila ya ugumu wo wote? Je, wanaweza kuonyesha matumizi sawa ya kifaa hicho?
- Je, aina gani ya mafunzo ya afya na usalama wa kikazi inayotolewa na/au kupewa SH/wafanya kazi?
- Kuna ushahidi gani wa kuonyesha mafunzo ya afya na usalama yaliyowahi kutolewa kwa SH/wafanya kazi (k.m. rekodi)?
- Je, kiwango cha utambuzi na maarifa ya hatari za kikazi miongoni mwa SH/wafanya kazi ni kipi (k.m. je, wanaweza kuonyesha matumizi salama ya vifaa)?
- Ni SH/wafanya kazi gani waliopewa mafunzo ya kutumia viuadudu?
- Pale ambapo viuadudu na/au kemikali mahsusi zinatajwa, ni ushauri gani (k.m. nyenzo za kuoga/kuosha zinazohitajika baada ya unyunyiziaji wa viuadudu) unaotolewa kwa SH/wafanya kazi?
- Je, wale wanaofanya kazi shambani humo huogea wapi baada ya kazi?
- Je, SH/wafanya kazi wanapata wapi maji ya kunywa (yaani kuna maji ya kunywa hapo shambani)?
- Je, SH/wafanya kazi wanahifadhi wapi vyakula vyao wanapofanya kazi shambani?
- Kuna aina gani za vyoo (vya jinsia zote) vya kutumiwa na SH/wafanya kazi?
- Je, kuna matayarisho gani kwenye mashamba ya SH ili kuhakikisha kuwa SH/wafanya kazi waja wazito au wanaonyonyesha hawafanyi kazi zilizo hatari kwao au kwa mtoto?
- Je, matayarisho haya maalumu kwa wanawake waja wazito na wanaonyonyesha yanawasilishwa kwao vipi?
- Je, wakati wa kazi, kina mama hunyonyesha watoto wao wapi?

C. 5 Ajira ya watoto haitatumika

- Je, wewe/SHE mna aina gani ya sera ya ajira ya watoto (k.m. umri wa chini zaidi, ujira, ulinzi dhidi ya hatari) katika mashamba ya SH?
- Je, matayarisho ya sera ya ajira ya watoto yanawasilishwa vipi kwa SH/wafanya kazi?
- Je, wewe/SHE mnahakikisha vipi kuwa sera ya ajira ya watoto inatekelezwa?
- Je, ni sehemu ipi ya watoto/vijana wanaofanya kazi kwenye mashamba ya SH inayohudhuria masomo shuleni?
- Je, ni sehemu ipi ya wale walio chini ya mkataba wa kufanya kazi kwenye mashamba ya SH iliyo na watoto/vijana?
- Je, ni muda gani ambao watoto/vijana wanaofanya kazi shambani wanahitaji ili kusafiri na kurudi kati ya mahali pa kazi na shuleni, na ni muda gani uliotumika shuleni?

C. 6 Mshahara wa kujikimu unalipwa

- Je, wewe/SHE hutumia kigezo gani katika kukokotoa gharama za uzalishaji zinazowiana na kulipa mshahara wa kujikimu kwa SH/wafanya kazi?
- Je, wewe/SHE unatoa mshahara ulio sawia au unaozidi gharama za uzalishaji kwa SH/wafanya kazi?
- Je, SH wameonyeshwa jinsi ya kukokotoa gharama zao za uzalishaji?
- Je, malipo ya kila kazi inayofanywa na wafanya kazi wa SH yanakubaliwa na kukokotolewa vipi?
- Je, wewe/SHE mna rekodi zinazoonyesha vile malipo/bei ya kila kazi zinakubaliwa/kukokotolewa, ikiwa ni pamoja na hali ambapo bei zinawekwa na mnada?
- Je, wewe/SHE mnajua vile rekodi za malipo ya SH/wafanya kazi zinawiana na zako/zao?
- Je, kuna ushahidi gani kuwa SH/wafanya kazi wanaelewa njia ya malipo na makato?
- Je, kuna kanuni zipi katika mkataba baina yako na SH (k.m. wingi na maelezo halisi ya bidhaa, kanuni za adhabu zinazotumiwa na mteja)?
- Kuna majukumu gani ya pamoja (k.m. kuhusiana na malipo na makato) yanayoelezwa katika mkataba baina ya SHE na wafanya kazi?
- Kuna tofauti gani baina ya aina ya mikataba inayowekewa wafanya kazi wa kiume na wa kike kutoka kwa SHE (k.m. mikataba inayozuia wanawake kazi wakiwa waja wazito)?
- Je, pande zote zinaheshimu masharti ya mikataba?
- Je, ukiukaji wa mikataba ni wa kiwango gani miongoni mwa: (tunatarajia makisio wala si tarakimu halisi)
  - kampuni yako/SHE _____%
  - SH _____%
  - Wafanya kazi _____%
- Je, SH wanapata pembejeo zao kutoka wapi (k.m. hapo kijijini au kutoka kwako)? Ikiwa unagawa pembejeo, je unawapa kwa bei ya uzalishaji?

C. 7 Masaa ya kazi hayazidishwi

- Je, SH/wafanya kazi wanalazimika kufanya kazi masaa ya ziada (yaani zaidi ya masaa 48 kwa wiki) mara ngapi (kwa mwaka mmoja)?
- Je, ni vipi viwango vya malipo ya ovataimu kwa wafanya kazi wa mashamba ya SH?
- Kuna ushahidi gani kuwa wafanya kazi wanaelewa viwango vya malipo yao ya ovataimu?
- Je, rekodi zinaonyesha malipo ya ovataimu yanayofaa yanayowiana na rekodi za SH/wafanya kazi?

- Je, kwa wastani wafanya kazi wanapata siku ngapi za mapumziko?
- Je, wewe/SHE mnahakikisha vipi kuwa ovataimu haiingilii majukumu ya uzazi ya SH/wafanya kazi?

C. 8 Hakuna ubaguzi wo wote unaofanywa?

- Je, maudhui ya sera ya SHE dhidi ya ubaguzi ni yapi (k.m. hakuna ubaguzi katika kuajiri, kupandisha cheo n.k kwa misingi ya ukabila, jinsia n.k)?
- Je, sera hiyo dhidi ya ubaguzi inawasilishwa vipi kwa wafanya kazi au SH wako?
- Je, ni kipi kiwango cha utambuzi na maarifa cha masharti ya sera dhidi ya ubaguzi miongoni mwa SH/wafanya kazi?
- Je, SH/wafanya kazi wanawake wanashiriki mara ngapi katika mafunzo?
- Je, kuna ushahidi kuwa SH/wafanya kazi wanaweza kushiriki katika mijadala bila kuogopa kubaguliwa au kuadhibiwa?
- Je, SH/wafanya kazi wanawake wanalipwa vipi kwa uzalishaji/kazi yao (k.m. moja kwa moja au sio moja kwa moja)?
- Je, tofauti ya ujira wanaolipwa wafanya kazi kutoka makabila madogo ni ipi?
- Je, kuna utaratibu gani wa kuhakikisha kuwa wafanya kazi wanawake hawazuiliwi kufanya kazi wakiwa waja wazito?
- Je, wewe/SHE mna sera gani ya kuajiri (k.m. nafasi sawa) katika mashamba ya SH?

C. 9 Ajira ya mara kwa mara inalolewa

- Je, habari kuhusu maagizo/ajira ya mara kwa mara inapitishwa vipi kwa SH/wafanya kazi?
- Je, SH wanapewa nakala za ilani kuhusiana na mabadiliko ya mahitaji (k.m. katika vituo vya kukusanya mazao)?
- Je, wafanya kazi wanajulishwa kuhusu uwezekano wa kuwepo kwa kazi baadaye inapowezekana?
- Je, wewe/SHE mna ufahamu mzuri kuhusu sheria za leba au ruzuku ya serikali?
- Je, ni sheria zipi za leba au ruzuku ya serikali zinazotawala uhusiano baina yako/SHE na SH/wafanya kazi?
- Je, unazingaria kiwango kipi cha utekelezaji wa sheria za leba na ruzuku ya serikali katika mashamba?
- Je, wafanya kazi wanafahamishwa vipi kuhusu hadhi yao ya ajira na kigezo cha kupewa hadhi hiyo?

C. 10 Hakuna utendaji wa kikatili au usio na huruma

- Je, SH/wafanya kazi huangalia vipi masharti ya kazi, shughuli za kuajiri na kazi (k.m. haina ukosefu wa heshima, vitisho wala kusumbuliwa)?
- Je, ni kwa kiasi gani ambapo wanawake katika mashamba wanasumbuliwa kimapenzi? Ikiwa ndivyo, mambo haya yanaelekea kufanyika wakati gani (k.m. ili wapate huduma/pembejeo au maagizo, ovataimu)?
- Je, ni mara ngapi wafanya kazi wanawake wanaripoti kuwa ovataimu inatumiwa kama kifaa cha kuwasumbua kimapenzi?

C. 11 Utaratibu wa malalamiko

- Je, wewe/SHE una mfumo gani wa kuwasilisha malalamiko?
- Je, wewe/SHE una maelezo ya mawasiliano ya wakaguzi wa serikali au ya njia huru za kushughulikia malalamiko kama vile chama cha wafanya kazi, shirika lisilo la kiserikali au chama cha SH/W?
- Je, SH/wafanya kazi wanajulishwa taratibu za kuwasilisha malalamiko zinazotolewa nawe/SHE?
- Je, SH/wafanya kazi wanaona kuwa wako huru kutumia mfumo huo wa kuwasilisha malalamiko

C. 12 Mfumo wa kanuni za utendaji

- Je, ni kipi kiwango cha utambuzi na maarifa ya masharti muhimu ya mfumo wa kimsingi wa kanuni za ETI na haki zake miongoni mwa SH/wafanya kazi??